

ya mfuko mmoja wa chakula cha kuku

Wauzaji wa vifaranga vya kuku waiangukia serikali

Na NASRA NASSORO (DSJ)

WAUZAJI wa vifaranga vya kuku wa nyama, wameiomba serikali kusitisha uingizaji wa vifaranga nchini kulinda soko la ndani kwa wazalishaji na wafugaji.

Akizungumza na gazeti hili juzi, mfugaji na muuzaji vifaranga, Shabani Abuu anayeishi Shekilango jijini Dar es Salaam, alisema hali ya soko la kuku ni mbaya kutokana na bei kushuka, huku bei ya vifaranga na chakula zikiendelea kupanda.

"Mimi nanunua vifaranga, nafuga na kuuza, ila changamoto kubwa hivi sasa huku sokoni, unanunua kifaranga sh. 2,500 unagharamia kwa sh. 6,000 na sokoni unauza sh. 5,500 hadi sh. 6,000, chakula cha kuku mfuko sh. 86,000 hadi sh. 90,000 na dawa zipo juu, tunaumia sana," alisema.

Alidai hali hiyo inasababishwa na uingizwaji wa vifaranga kwa njia za magendo kutoka nchini Uganda na Malawi. Abuu alisema mwanzo alikuwa anauza kuku maboksi 50 yenye vifaranga 6,000, ila hivi sasa anauza maboksi matano kwa mwezi, hali ambayo inamrudisha nyuma kimaisha.

Kwa upande wake, muuzaji Nadhifu Masemwa, aliomba serikali kuwachukulia hatua watu wanaoingiza vifaranga kwa njia ya magendo ambayo alisema inaua soko la ndani.

"Unaporuhusu mtu aingize vifaranga maboksi 500 ni lazima soko la ndani liathirike, hivyo tunaomba serikali iangalie jambo hili, kwani wanaumia ni wazalishaji wa ndani," alisema.

Naye, mfugaji Pangawe Lucas, alisema hatua za haraka zisipochukuliwa, wajasiriamali wataathirika na kuuza mitaji yao.

"Nilikuwa nafuga na kuuza kuku 3,600 kwa mwezi, ila kwa sasa hata 1,000 hawafiki na mtaji unaendelea kuporomoka," alisema.

Mkazi wa Mabibo, Dar es Salaam, Said Abdallah alisema anapitia wakati mgumu kutokana na biashara kuyumba katika miezi ya hivi karibuni.

"Mimi ni wakala wa vifaranga kutoka Kampuni ya Organia, hali ya biashara ni mbaya, nauza kuku wenye wiki nane yaani miezi miwili kutoka mwezi mmoja wa awali, ni gharama kubwa kuwatunza. Nilikuwa nauza kuku 4,000 kwa mwezi lakini kwa hivi sasa tunabahatisha," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Kuku wa Nyama Tanzania (TABROFA), Aloyce Makoye, alisema biashara ya kuku wa nyama na vifaranga imeharibika.

"Kuna mafuriko ya kuku wa nyama wanaotakiwa kuingizwa sokoni, hali ambayo imeshusha bei na matokeo yake ni mitaji ya wafugaji kutetereka. Sisi tunahisi kuna mwanya unatumika kuingiza kuku kwa njia ya

panya, tunaomba mamlaka zichukue hatua, kwani tunaenda kufilisika," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kuzalisha Vifaranga ya Organia, Albert Momdjian, alisema wanapata uchungu kwa kinachoendelea katika sekta ya kuku nchini.

Momdjian alidai baadhi ya watu wamekuwa wakikwamisha ukuaji wa sekta hiyo jambo ambalo alisisitiza hawatakubali liendelee kuharibu jamii ya wafugaji wa Kitanzania.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo ambaye ndiye mtoaji vibali vya kuingiza mifugo ikiwemo vifaranga, Profesa Hezron Nonga, alikanusha taarifa za wizara kutoa vibali vipya vya uingizaji wa vifaranga nchini.

Profesa Nonga alisema hadi hivi sasa kampuni zinazoingiza vifaranga ni mbili ambazo ni Wolowolo Animal Care Center na The One Agro Enterprise zilizopata vibali kuanzia mwaka jana na vifaranga vinavyoingizwa ni katika kumalizia maombi yao za zamani.

"Hizi kampuni ziliomba vibali katika kipindi ambacho nchi ilikuwa na changamoto ya uhaba wa vifaranga, ambapo The One Agro Enterprise imeruhusiwa kuingiza vifaranga 494,000 kutoka Uganda na Wolowolo vifaranga 150,000 kutoka Malawi na mwisho wa kuingiza ilikuwa ni Januari 15, mwaka huu," alisema.

ZIMAMOTO